

Krismasi Na Pasaka

Sehemu mbili katika habari ile ile

Wakati wa kipindi cha furaha cha Krismasi, kuzaliwa kwa Kristo, hujaa mapambo ya taa zing'azoo, sherehe, na Santa Claus (Baba Krismasi), Vivyo hivyo, katika Pasaka, kifo chake, kuzikwa kwake na kufufuka kwake kwa kawaida hujawa na mitindo ya nguo, michezo na chakula cha pekee cha Pasaka

Kwa sababu hiyo, watu wengi hawajui umuhimu wa matukio haya mawili katika maisha ya Yesu Kristo. Watu wengi hawaoni muunganiko wa kuzaliwa kwake katika hori la ng'ombe na kifo chake pale msalabani, na hivyo wanakosa umuhimu wake.

Hebu tujikumbushe juu ya muunganiko huu muhimu. Itayafanya haya matukio mawili kuwa na maana zaidi kwako.

Miaka mingi kabla ya kuzaliwa kwa Kristo, Mungu alisema, « Bikira atachukua mimba, atazaa mtoto mwanamume, naye atamwita jina lake Imanueli (Mungu pamoja nasi) ». Kuzaliwa na bikira kwa Kristo ilikuwa ni utimilifu wa unabii na kuthibitisha kuwa ndiye Mwokozi Mungu aliyeahidi.

Licha ya jinsi picha na sanamu zake za kidini zinavyo mwonyesha, Yesu hakubakia mtoto mchanga. Alikua na kuwa mtu mzima ambaye alikufa kwenye msalaba pale Kalvari. Kusulubiwa kwake halikuwa jambo la ajabu kwa Yesu, kama alivyokuwa amewaeleza wanafunzi wake mara kwa mara ya kuwa ni lazima angelikufa ili awe Mwokozi wa wenye dhambi. (Mat. 16 :21). Biblia inasema, « Kristo alikufa kwa ajili ya dhambi zetu, kama yanavyo maandiko ». (1Kor.15 :3). Kifo chake, kama kuzaliwa kwake, ilikuwa ni utimilifu wa unabii uliokuwa umetolewa miaka mingi kabla. (Isa. 53 :1-9).

Habari za kushangaza zaidi katika biblia ni kuwa, Kristo hakufa tu kwa ajili ya dhambi zetu, lakini pia « alifufuka siku ya tatu » kama alivyokuwa ameahidi kabla ya kifo chake. (Yoh. 2 :19-22). Kufufuka kwake ilikuwa ni muhuri wa uthibitisho wa kuwa dhabihu kamili kwa ajili ya dhambi zetu. (Heb. 10 :12).

Mungu hakuhitaji wewe uweke imani yako kwa mtoto mchanga, au

kwa mtu mzuri aliyetenda miujiza. Anakutaka uweke imani yako kwa Mwanawe wa milele ambaye aliuchukua ubinadamu katika hori kule Bethlehemu na miaka takriban thelathini baadaye akaenda msalabani Kalvari kuibeba hukumu ya Mungu kwa ajili ya dhambi zetu. Yeye ambaye baada ya siku tatu alifufuka kutoka kwa wafu, akapaa mbinguni, na leo yu hai katika mkono wa kuume wa Mungu. (Mdo. 2 :36).

Je, ulishawahi kuunganisha kati ya Krismasi na Pasaka ? Umeona ya kuwa Kristo alikuja humu duniani kwa njia ya kuzaliwa na bikira na kwenda msalabani kubeba ghadhabu ya Mungu juu ya dhambi ZAKO ? Kama utakiri dhambi zako na kumkubali Yesu Kristo kama Mwokozi wako unaweza kuijua furaha ya kusamehewa dhambi zako zote na kuwa na uzima wa milele. (Yoh. 5 :24 ; 1Yoh 5 :13).

Soma biblia yako na uone jinsi unavyoweza kuokolewa kutoka katika hukumu ya Mungu kwa njia ya imani katika Yesu Kristo. Tunakushauri uanze kusoma injili ya Yohana.

“Kwa maana jinsi hii Mungu aliupenda ulimwengu, hata akamtoa Mwanawe wa pekee, ili kila mtu amwaminiye asipotee, bali awe na uzima wa milele” (Yoh. 3:16).

« Na sisi tumeona na kushuhudia ya kuwa Baba amemtuma Mwana kuwa Mwokozi wa ulimwengu ». (1Yoh. 4 :14)

« Utamwita jina lake Yesu, maana yeye ndiye atakayewaokoa watu wake na dhambi zao ». (Mat. 1 :21)

« Ni neno la kuaminiwa tena lastahili kukubalika kabisa ya kwamba Kristo Yesu alikuja ulimwenguni awaokoe wenye dhambi ». (1Tim 1 :15).

« Mwamini Bwana Yesu nawe utaokoka ». (Mdo. 16 :31)

« Kwa maana mmeokolewa kwa neema kwa njia ya imani, ambayo hiyo haitokani na nafsi zenu, ni kipawa cha Mungu ; wala si kwa matendo mtu awaye yote asije akajisifu ». (Efe. 2 :8-9)

Spread the Word,
P.O. Box 7046
York, PA 1704.